

TANGAZO LA SERIKALI NA. 582 la tarehe 18-12-2015

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA

(SURA YA 290)

SHERIA NDOGO

(Zimetungwa chini ya kifungu cha 16 (1) na 7 (1))

SHERIA NDOGO ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA GEITA ZA (ADA NA USHURU) (MAREKEBISHO) ZA MWAKA, 2015

Jina na tarehe ya Kuanza kutumika

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za Halmashauri ya Wilaya ya Geita za (Ada na Ushuru) Marekebisho za mwaka, 2015 na zitasomwa pamoja na Sheria Ndogo za Halmashauri ya Wilaya ya Geita za (Ada na Ushuru) za mwaka 2008, na zitaanza kutumika mara baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali;

Eneo la kutumika

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika pamoja na Sheria Ndogo za Ada na Ushuru za Halmashauri ya Wilaya ya Geita za mwaka 2008. na zitatumika katika eneo lote lililopo chini ya Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Geita;

(GN 301 la tarehe 14/11/2008)

3. Jedwali A linafanyiwa marekebisho katika sehemu mbalimbali kama ifuatavyo;

SEHEMU A

Ada ya kuweka vibao vya Matangazo

(1). Kipengele (I) (a) kwa kufuta maneno “Sh.500/= kwa kila sentimeta 100 za mraba” na badala yake isomeke “Sh. 20,000/= kwa kila meta 1 ya mraba”.

Katika kipengele (I)(b) kwa kufuta maeneo “Sh. 1,500/= kwa kila sentimeta 100 za mraba na badala yake isomeke “Sh.40,000/= kwa kila meta moja ya mraba”.

Katika kipengele (II) (a) kwa kufuta maneno “Sh. 1,000/= kwa @ ng’ombe na badala yake isomeke “Sh. 5,000/=” @ ng’ombe.

Ushuru wa mifugo

Katika kipengele (II) (b) kwa kufuta maneno Sh.500 @ mbuzi au kondoo” na badala yake isomeke “Sh. 1,500/= @ mbuzi au kondoo”.

SEHEMU B

Ushuru wa

(3) Ada za Maegesho na huduma za usafirishaji zimefanyiwa marekebisho kama ifuatavyo:

kuegesha
magari kituo
kikuu cha
mabasi

- (a) Katika kipengele (i) (a) kwa kufuta maneno Sh. 1,000/= na badala yake isomeke “Sh. 3,000/=
- (b) Katika kipengele (i) (b) kwa kufuta maneno Sh. 500/= na badala yake isomeke “Sh.2,500/=”
- (c) Katika kipengele (i) (c) kwa kufuta maneno Sh. 200/=” na badala yake isomeke “Sh. 1,000/=”.

SEHEMU C

Kodi ya
kutumia
mali za
Halmashauri

(4) Ada ya Ukumbi wa Halmashauri imefanyiwa marekebisha kama ifuatavyo:-

- (a) Katika sehemu “C” kipengele (a) kwa kufuta maneno “Sh. 100,000/= kwa siku” na badala yake isomeke “Sh. 150,000/= kwa siku”;
- (b) Katika sehemu “C” kipengele (c) (i) na (ii) kwa kufuta maneno “Sh. 200/= kwa siku” na badala yake isomeke “Sh. 300/=” na kufuta shilingi 200/= kwa siku na badala yake isomeke “Sh.400/= kwa siku”;
- (c) Katika sehemu “C” kipengele (d) (i) kwa kufuta neno “Sh. 100/= kwa siku “ na badala yake isomeke “Sh. 200/= kwa siku”.

SEHEMU D

Ada ya
huduma ya
machingio

(5) Ada ya kuchinja mifugo machinjioni imefanyiwa marekebisha kama ifuatavyo:

Katika sehemu “D” kipengele (a) (i) kwa kufuta maneno “Sh. 1,600/=” na badala yake isomeke “Sh. 3,000/=”.
Katika sehemu “D” kipengele (a) (ii) kwa kufuta maneno “Sh 800/=” na badala yake isomeke “Sh 1,000/=”.

SEHEMU F

Ushuru kwa
shughuli za
uvuvi

(6) Ushuru kwa shughuli za uvuvi umefanyiwa marekebisha kama ifuatavyo:-

Sheria ndogo kuu inafanyiwa marekebisha katika Jedwali, sehemu “F” kipengele (a) (v) kwa kufuta neno sh.1,000 na badala yake isomeke sh. 10,000 kwa kila kilo moja Sehemu “F” neno Sh. 10 @ kg na badala yake isomeke “sh. 150 kwa kila kilo moja”

SEHEMU H

- (d) Ada ya Usafishaji (site clearance) imefanyiwa marekebisha kwa

kufuta vipengele vyote kuanzia kupengele cha (i), (ii), (iii) na (iv).

SEHEMU I

Ushuru wa
marudio ya
mchanga
wenye
dhahabu

(7) Sheria Ndogo ya ada na ushuru inafanyiwa marekebisho katika jedwali kwa kuongeza sehemu I na nyongeza yenye tozo mpya ya ushuru wa marudio ya mchanga wenye dhahabu na miundo mbinu ya kuchakata dhahabu.

I (a) kampuni zinazojishughulisha na marudio ya dhahabu zitalipa ushuru wa marudio wa kiasi cha shilingi milioni tano tu [5,000,000/=] kwa kila mwaka.

I (b) ushuru wa mwalo utakuwa shilingi elfu kumi tu [10,000/=] kwa kila mwezi.

I (c) ushuru wa karasha utakuwa shilingi elfu kumi tu [10,000] kwa kila mwezi.

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Geita imewekwa katika Sheria Ndogo hizi kufuatia azimio lililopitishwa kwenye mkutano wa Halmashauri uliofanyika tarehe 29 Aprili, 2015 na kubandikwa mbele ya:-



.....
ALIA. KIDWAKA

Mkurugenzi Mtendaji

Halmashauri ya Wilaya ya Geita

NAKUBALI,

Dodoma,
3 Novemba, 2015

.....
ELISHA. H. LUPUGA

Mwenyekiti

Halmashauri ya Wilaya ya Geita